# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
## JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI

## TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA

Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kifungu cha 14(4) cha Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Sura ya 427, kikisomwa pamoja na Kanuni ya 5(1) ya Kanuni za Utumishi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji za mwaka 2008; anatangaza nafasi za ajira ngazi ya Konstebo wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa vijana wenye sifa zifuatazo: -

**1. Elimu ya Kidato cha Nne**

**Sifa za mwombaji.**

a) Awe raia wa Tanzania kwa kuzaliwa
b) Awe na Kitambulisho cha Taifa au Namba ya Utambulisho iliyotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho (NIDA)
c) Awe na afya njema kimwili na kiakili
d) Asiwe na kumbukumbu za uhalifu
e) Awe hajaoa au kuolewa
f) Asiwe na alama za kuchorwa mwilini (Tattoos)
g) Awe hajawahi kutumia aina yoyote ya madawa ya kulevya
h) Awe tayari kuhudhuria mafunzo ya taaluma ya Zimamoto na Uokoaji
i) Awe hajawahi kuajiriwa serikalini
j) Awe mwenye urefu usiopungua futi 5.7 kwa mwanaume na futi 5.4 kwa mwanamke
k) Awe tayari kujigharamia katika hatua zote za usaili endapo ataitwa
l) Awe tayari kufanyakazi popote atakapopangiwa baada ya kumaliza mafunzo
m) Umri kuanzia miaka 18 hadi 25.

2. **Elimu ya Kidato cha Nne au Sita.**

Madereva wa magari makubwa, Wauguzi ngazi ya Stashahada, taaluma za Zimamoto na Uokoaji, Matabibu ngazi ya Stashahada, Mafundi mchundo wa magari, wazamiaji na waogeleaji, Wanamichezo, Brass band, Waandishi Waendesha Ofisi, TEHAMA ngazi ya Stashahada na mafundi umeme wa ndege ngazi ya Stashahada.

**Sifa za mwombaji.**

a) Sifa zote zilizoainishwa kwenye Aya ya 1 (a hadi I)
b) Umri kuanzia miaka 18 hadi 28
c) Wazamiaji na waogeleaji watafanyiwa uhakiki kwa vitendo
d) Madereva, awe na leseni daraja E (watakaoitwa kwenye Usaili watafanyiwa uhakiki kwa vitendo kuendesha magari makubwa).

3. **Elimu ya Shahada.**

Wahandisi Bahari, TEHAMA, Wahandisi wa Ndege, Wakadiriaji Majenzi (QS), Sheria (waliohitimu shule ya sheria kwa vitendo), Mafuta na gesi, Wahandisi ujenzi, Wahandisi mitambo na Wahandisi umeme.

**Sifa za mwombaji.**

a) Sifa zote zilizoainishwa kwenye Aya ya 1 (a hadi I)
b) Umri kuanzia miaka 18 hadi 28.

4. **Namna ya kuomba.**

Maombi yote yawasilishwe kupitia mfumo wa ajira wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji unaopatikana kupitia kikoa cha **https://ajira.zimamoto.go.tz** mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **03 Desemba, 2025.**

Mwombaji aambatishe kwenye mfumo nyaraka zifuatazo: -

a) Barua ya maombi iliyoandikwa kwa mkono na mwombaji kwenda kwa,
Kamishna Jenerali,
Jeshi la Zimamoto na Uokoaji,
1 Mtaa wa Zimamoto,
S.L.P 1509,
**41102 DODOMA.**
b) Fomu ya uthibitisho wa siha njema kutoka kwa mganga wa serikali

c) Nakala ya Kitambulisho cha NIDA au namba.

d) Namba ya mtihani wa Kidato cha Nne

e) Namba ya mtihani wa Kidato cha Sita

f) Namba ya vyeti vya taaluma kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada

g) Namba ya kumbukumbu ya barua ya Utambulisho kutoka kwa Afisa mtendaji wa Kijiji/Mtaa (Kupitia mfumo wa NaPA).

**Zingatia:**

a) Nakala za vyeti vingine kama vipo mbali na vilivyotajwa kwenye aya ya 4(d),(e) na (f) viambatishwe vikiwa vimethibitishwa na Kamishna wa viapo au hakimu

b) Barua zitakazowasilishwa kwa njia ya posta, mkono au kwa barua pepe **hazitapokelewa**

c) Waombaji wote waandike namba za simu kwenye barua zao za maombi

d) Mwombaji atakayewasilisha nyaraka za kughushi au taarifa za uwongo atachukuliwa hatua za kisheria

e) Mwombaji atapimwa tena afya ya mwili na akili akifika Chuoni.

limetolewa na;

CGF

**19 Novemba, 2025**

John W. Masunga
**KAMISHNA JENERALI**
**JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**